

ST.THERESIA GIRLS SECONDARY SCHOOL PARTICULARS

Jina la shule:- ST.THERESIA GIRLS SECONDARY SCHOOL.

Mwaka wa kuanzishwa:- 2007.

Namba ya usajili:- S2536.

Mmiliki:- SHIRIKA LA MASISTA WA MARIA MTAKATIFU MALKIA WA AFRIKA (M.M.M.M.A).

Mkurugenzi:- Sr. EDITRUDA MBEGU.

Meneja: Sr. LUCY TENDEZA

Anuani:- S.L.P 38.

Namba ya simu ya mkuu wa shule:- 0755248837.

Namba ya simu ya makamu wa mkuu wa shule:- 0764200620.

Namba ya simu ya mhasibu wa shule:- 0755557315.

Barua pepe:-st.theresiasecondary@yahoo.com.

Aina ya shule:- Shule ya bweni pekee.

Aina ya wanafunzi:- Wanafunzi wa kike tu

Idadi ya wanafunzi:- 305 baada ya kidato cha nne kumaliza Novemba 2023

Idadi ya walimu:- Ke-05

Me-13

Jumla kuu ya walimu:- 18

HISTORIA FUPI YA SHULE

CHIMBUKO LA KUENZISHWA SHULE.

Shirika la Masista wa Maria Mtakatifu Malkia wa Afrika (MMMMMA) lilibaini kuwa katika Mkoa wa Rukwa hususani Jimbo Katoliki la Sumbwanga watoto wa kiume hupewa nafasi kubwa zaidi katika kupata elimu ikilinganishwa na watoto wa kike.

Ili kuleta uwiano mzuri kati ya watoto wa kiume na wa kike katika kupata elimu, shirika lilikusudia kuanzisha shule mahususi kwa ajili ya wasichana.

Mpango wa awali ulikuwa kujenga shule itakayotoa elimu kwa wasichana kuanzia

- Chekechea
- Msingi
- Sekondari
- Chuo.

Shirika lilifanikiwa kupata eneo hili lililojulikana kama “Mama Educational Centre” kwa bahati mbaya eneo hili halikutosheleza kujenga majengo kwa ajili ya shule ya Chekechea, Msingi , Sekondari hadi Chuo.

Hivyo iliamuliwa kuanza na shule ya sekondari, kwa sababu idadi kubwa ya watoto wa kike wanaweza kupata elimu ya msingi.

Shule iliwekwa chini ya usimamizi wa Mtakatifu Therezia na hivyo kujulikana kama shule ya sekondari ya Mt. Teresia.

Ujenzi wa majengo ya shule ulianza mwaka 2005 kwa msaada wa wafadhili mbalimbali kutoka

- Italia
- Ujerumani
- Uholanzi

Shule ilianza rasmi mwaka 2007 ikiwa na idadi ya wanafunzi 87 na walimu wane (4). Mpaka sasa shule ina idadi ya wanafunzi 305 kuanzia kidato cha kwanza hadi cha sita.

Shule hii inamilikiwa na Shirika la **Masista wa Maria Mtakatifu Malkia wa Africa (M.M.M.M.A)**.

Shule hii ilianzishwa na shirika, kwa kujiegemeza kwenye kauli mbiu ya “**Ukimuelimisha mwanamke umeelimisha jamii nzima**”

Hadi hivi sasa shule hii ndiyo shule pekee katika manispaa ya mji wa Sumbawanga na mkoa wa Rukwa kwa ujumla inayotoa elimu kwa wanafunzi wa kike wanaokaa bweni tu kuanzia kidato cha kwanza hadi kidato cha sita.

Aidha idadi ya majengo imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka yakiwepo madarasa, maabara na mabweni.

MAENDELEO YA KITAALUMA:

MATOKEO YA MITIHANI KIDATO CHA PILI KUANZIA MWAKA 2019-2022

MWAKA	DARAJA					JUMLA YA WANAFUNZI	GPA
	I	II	III	IV	0		
2019	34	36	40	13	0	123	
2020	48	25	27	16	0	116	
2021	31	23	15	12	0	81	
2022	21	14	21	28	3	87	3.1690

MATOKEO YA MITIHANI KIDATO CHA NNE KUANZIA MWAKA 2019-2022

MWAKA	DARAJA					JUMLA YA WANAFUNZI	GPA
	I	II	III	IV	0		
2019	10	48	43	7	0	108	2.8545
2020	33	35	32	2	1	102	2.5550
2021	13	67	38	4	0	122	2.7380
2022	9	49	35	26	0	119	3.0137

MATOKEO YA MITIHANI KIDATO CHA SITA KUANZIA MWAKA 2019-2023

MWAKA	DARAJA					JUMLA YA WANAFUNZI	GPA
	I	II	III	IV	0		
2019	2	9	9	0	0	20	3.1750
2020	1	5	6	1	0	13	3.4615
2021	2	13	4	0	0	19	2.9386
2022	2	3	2	0	0	7	2.7857
2023	1	5	1	0	0	7	2.8571

CHANGAMOTO:

Shule bado ina uhaba wa majengo yafuatayo

-Ukumbi wa mikutano, Maktaba na jingo moja la maabara ya sayansi.

MIPANGO YA BAADAE

Shule bado ina mikakati ya kutimiza lengo lake kuu la kutoa elimu kwa wasichana kuanzia O level ____A level ____Chuo.

MATAMANIO:

Shule yetu ina matamanio makubwa ya kufanya vizuri katika kuondoa matatizo na changamoto katika:

- (i) Kuwa na vitabu vya kutosha vya kufundishia na kujifunzia (yaani vya kiada na ziada) kwa masomo yote.
- (ii) Kuwa na vifaa vya kutosha vya maabala ili kuwawezesha wanafunzi kufanya majaribio mbalimbali kwa vitendo.
- (iii) Kuendelea kuwaandaa walimu bora na waliojitoa kufundisha kwa kuwapa mafunzo mbalimbali katika ufundishaji na kuwapa elimu na uzoefu kwa masomo yote.







“Pamoja Tunajenga Taifa Letu”

SR. KAROLINE T. KILIANI

MKUU WA SHULE